## <u>“Tega sikio ujifunze” Elimu ya Kawaida; EPISODE 5</u>

**“Kwanini Mayai huwa magumu na Viazi kuwa laini vinapopikwa”?**

**Mwandhishi: Lydia Heller**
**Mwelekezi : Maja Dreyer**
**Tafsiri : Eric Ponda**

**<u>Wahusika:</u>**

**Mtangazaji**
**Jenny Msichana (14)**
**Jack Mvulana (15)**
**Mamake Jack Bi. Mulokozi**
**Wengine 3-5 Watoto na watu wazima**

<u>Sauti</u>
Simu ikilia na kupokelewa na Jack
Hatua zikitokomea kwa haraka
Mlango ukibishwa
; ukifunguliwa
Sufuria zikigongana
Mfereji ukifunguliwa
Maji yakichotwa kwenye sufuria
Maji yakichemka
Sufuria mayai vikianguka sakafuni
Sauti ya kufagia na kupangusa
Sauti ya Redio kwa mbali
Mayai yaliyochemshwa na kuambuliwa.
Watu wakipiga miguu sakafuni,wakicheka, kuangukia kadhalika

INTRO (Mtangazaji)

Hujambo msikilizaji na karibu katika kisa kingine cha “Kujifunza kwa Kusikiliza” katika mfululizo wa vipindi kuhusu elimu ya kawaida ya mambo ya kila siku. Leo tutasikiliza kile kinachotokea wakati mayai na viazi vinapopikwa. Unaweza kuchukulia kuwa ni jambo la kawaida lakini mambo haya ni kuhusu sayansi, yaani fisikia, baiolojia na kemia. Hivi sasa Jenny haweza hata kupika kimanda bila ya kufikiria kisayansi. Hali hiyo ni tangu

alipomwalika Jack kwa chakula cha mchana na akaibadilisha familia nzima ya Jenny kuwa moleculi za proteini. Alikuwa akijaribu kuwaonyesha ufahamu wake kuhusu ni kwa nini mayai hugeuka kuwa magumu yanapopikwa na viazi kuwa laini. Na hayo yote ni katika kumfariji Jenny kwa kusahau mwaliko wake.

---

1. Scene

*(Simu ya mkono inalia, Jack anajibu)*

**Jack:** "Jack hapa, halo? Ala Jenny, vipi? *(akigutuka kidogo,kana kwamba kafumaniwa)* Mkutano wetu? Ah, um, ndio, ndio, ni sawa. Oh, leo? Hapana sikuwa nimesahau, la hasha. Tayari ulikuwa ukinisubiri? Tayari nusu saausu saa? *(akiguguna)* Niko njiani. Nitafika wakati wowote sasa…Bye.

*Hatua za haraha-haraka*

*Mlango unabishwa, mlango unafunguliwa.*

**Jenny***:(kwa hasira*) "Hatimaye! Namekualika kwa chakula cha mchana, wajua natatizika kwa wiki kadhaa sijui nipike nini, nimekwenda dukani kununua chakula na bado nahangaika jikoni! Na wewe ni kumelala tu! .

**Jack:** *(akimbembeleza)* Ah Jenny, pole sana, *(akinusanusa)* Kwani tunakula nini?

**Jenny:** *(bayana)* "Mayai ya kuchemsha."

**Jack:** "Mayai ya kuchemsha?"

**Jenny:** *( akiona haya)* "Kwa kweli huo ndio upishi niujuao. Na hata hayajakuwa tayari."

**Jack:** *( akiwa amechanganyikiwa, na kuona aibu kwa kusahau mwaliko huo, hakutaka kumudhi Jenny)*"Ooh, usijali. Nitakusaidia. Wataka nifanye nini?"

**Jenny:** *(akirejelea hali yake ya furaha)*“Basi hapa kuna sufuria na maji yako pale’

*Sufuria zikigongana, mifereji ikifunguliwa na sufuria ikitiwa maji.*

**Jack:** “Sasa tayari nimetia maji sufuriani, kuiweka jikoni na kuliwasha jiko. Sasa tusubiri…

*(Maji yakichemka)*

**Jenny:** “Sasa maji tayari. Tutie mayai.”

**Jack:** *( akipaza sauti kwa hasira)* “Ngoja kwanza Jenny!”

*(Jenny ameshtuka. Sufuria mayai yanaanguka sakafuni kwa sauti kubw)*

**Jack***:(akiongea kama mtaalamu wa sayansi kana kwamba kila mtu anaelewa anasema nini)*“Ikiwa utatia mayai kwenye maji ya moto, unaharibu mpangilio wa molecule za protein kwenye mayai. Maji moto huvunja molecule hizo za protein, na kuzifanya kushikana na protein nyingine. Katika hali hiyo zinaskuma maji ambayo huzunguka kila molecule wakati yai lingali maji-maji. Hiyo ndiyo sababu yai hugeuka na kuwa gumu. Na yai hilo haliwezi kugeuzwa tena kuwa maji-maji, asilani.”

*(sauti ya vitu kuanguka).*

**Jenny:** *(ashtuka…haelewi)* “Nini?’

**Jack:** *(hana haraka)*“Nimesema kuwa mayai hayo yatakuwa magumu na yatabakia vivyo hivyo”

*( apumua kidogo halafu kwa hasira kubwa)*

**Jenny:** *(akiwa ameudhika)* “SIKILIZA!, WEWE MWENDA WAZIMU NINI? Angalia balaa yote hii. Ikiwa hutanisaidia kufagia, basi urafiki wetu kwisha na nitatafuta rafiki mwengine thabiti”.

*(akifagia na kupangusa)*

**Jenny:** *(akivuta pumzi ndefu)* " Sasa niambie,kwa nini mayai yanakuwa magumu yanapopikwa?

**MUZIKI…..**

SURA YA PILI

*(Yai likivunjwa huku sauti ya redio chini kwa chini)*

**Jenny***:( akiwa amefundira na, akitafuna)* "Sasa profesa? Nasubiri! Kwa nini mayai huwa magumu yanapopikwa?"

**Jack:** *(anabugia yai kanwani, atafuna na kumiza)* Ni kwa sababu yametengezwa kwa protein, ….molecule za protein!.

**Jenny;** "Ohhh, hapana. Usianze tena, tafadhali. Unahakika? Wewe ummesikia tu na huna uhakikika wa chochote, na sasa wajifanya mtaalamu.

**Jack***:(anamkatiza, kwa uhakika)* "La, na uhakika wa ninachosema. Nilikuwa nikitazama kipindi kwenye Televisheni kuhusu sehemu nyeupe ya mayai na protein.

**Jenny:** "nimesema mimi!. Umesikia tu habari hizo mahali lakini huna uhakika."

**Jack:** "Oh Jenny, wacha utundu, si umwite kakako mdogo, dadako na nyanyako na majirani huku jikoni…. Yaani yeyote yule anayeweza kuja…."

**Jenny:** "Mama, Nyanya! Freddy! Hebu njooni hapa kidogo"

*(Sauti za watoto na watu wazima zasikika)*

**Jack:** “Mumekuja haraka. Hamjambo? Habari Bibi Mulokozi! Nawaahidi kwamba nilichowaitia hakitachukua muda mrefu, tutaigiza jinsi molecule za protein zinavyokuwa katika hali tofauti-tofauti, na kwa sasa ni vile zinavyokuwa kwenye mazingira ya joto.”

**Jenny:** *(akiwa ameudhika huku akionya)* “Wacha mambo mengi Ja..a..cck.”

**Jack:** “Sawa, sawa. Hakuna shida. Nataka muchukulie hiki chumba ni mfano tu wa yai bichi, na sisi ni ile sehemu nyeupe ya yai…na ikiwa mwataka kujua sehemu hiyo nyeupe kisayansi inaitwa albumen. Kila mmoja wetu ni molecule moja ya protein…chembe-chembe ndogo ya ule wepe wa yai. Chembe chembe zote zimeungana. Kwa mfano, fikiria kwamba kidole chako kinamgusa jirani yako. *(Awaagiza)*Mguse jirani yako kwa kidole chako kidogo.”

*( Sauti za watu na vicheko….."Sawa")*

**Jack:** “Sawa, sasa sisi ni mchnganyiko kama vile molecule za protein katika yai bichi, na tayari tumeanza kutokwa jasho na maji yametuzunguka. Weupe wa yai ni mchnganyiko mzito kwa sababu chembe chembe za protein zake hazikushakamana. Lakini sasa fikiria kwamba sakafu inaanza kupata moto.Kwa mfano kama tungetupwa ndani a maji moto kama vile weupe wa yai, tungekuwaje? Si tutaanza kutapatapa, kugeuka-kuruka-ruka,*(akionyesha mfano)* kukimbia, haraka-haraka.

*(Milio ya watu kupiga miguu sakafuni, wakiongea, wakipiga kelele, wakicheka)* “Aaah siwezi kuhimili zaidi!!” “Nitaanguka” “Niwache” Mimi pia naanguka” Kuwa mwangalifu” na kdahalika

**Jack:** *(Sauti haimtoki vizuri, amelaliwa na wengine.)* “Mnafikiri nini kitatokea? Sasa sio kugusana tena, tumebanwa pamoja sakafuni kama ugali.*(anajikwamua kutokana na miili ya watu)* Jenny, hivyo ndivyo inavyotendeka wakati yai likipikwa”

**MUZIKI……**

*(Sauti za watu, kicheko, kulalamika, viti vinasukumwa, nguo zalainishwa. Walioko wanajaribu kuelewa kilichotendeka)*

**Jenny:** *(akiwa na wasi wasi na woga)* "Mama, wacha nikusaidie. Umeumia mahali popote. Pole sana, sikujua huyu Jack mtundu angefanya hivi."

**Mama Jenny:** *(akinung'unika,na kumkatiza Jenny)* "Niko salama salimini. *(akijinyoosha)* Sikuvunjika mahali. Kwa kweli haikuwa mbaya sana.—si kila siku mtu hunambia kuwa mimi ni molecule ya protein. Lakini Jack?"

**Jack:** *(akiwa na woga)*Naam, Bibi Mulokozi."

**Mama Jenny:** "Sielewi ni kwanini, pia viazi vina protein, lakini haviwi vigumu vikipikwa, na badala yake vinakuwa laini!... ni kwanini.?"

**Jack:** *(Woga ukiwa umemtoka)* Aaha… najua pia! Tunaweza kufanya zoezi lingine…."

*(Hatua za haraka, viti vikisukumwa,watu wanatoka, wakizungumza).* "Inanibidi niende" "Sina wakati zaidi" "Tuonane baadaye Jack" na kadhalika.

**Jack:** *(kwa mshangao)* "Lakini Bibi Mulokozi, mbona wameondoka ghafla hivyo?

**Jenny:** "Labda wana kikao kingine chambilecho mchezo wa kuigiza wa chembe chembe za tembe ya dawa ya kichwa.*(akiwa ameudhika)* Wewe Jack unaweza kuibisha Mtu!"

**Jack***:* *( pia akiwa ameudhika)* "Hata hivyo mama yako ameuliza kuhusu viazi. Si afadhali nikueleze wewe, au huna haja ya kujua?"

**Jenny:** (*kwa uchovu)* “Ikiwa ni lazima, endelea, lakini safari hii hakuna zoezi”

**Jack:** “Kwa kweli mama yako hakukosea, kuna protein kwenye viazi lakini wanga ndio mwingi zaidi na wakati mwanga ukipikwa,viazi hivyo hunyonya maji zaidi na hivyo kuwa laini. Viazi vikipikwa kwa muda mrefu zaidi vinapogeuka kuwa kama ugali.”

**Jenny:** “Kwa sababu vina wanga mwingi?”

**Jack:** “”Kabisa! *(akisitasita)* Sasa umeacha kunikasirikia, sio? Kesho njoo kwetu kwa chakula cha mchana lakini si cha mayai ya kuchemsha.

**Mwisho….**

*Mlango unabishwa,kasha unafunguliwa.*

**Jack:** *(akijifanya mtu mzima)* “Nilidhani hutakuja!. Mbona imekuchukua muda mrefu hivyo? Nimekuwa nikingangana jikoni peke yangu kwa muda mrefu”

**Jenny:** Aah Jack, pole sana. *(Ananusa hewa,)* Kwani unapika nini? Kinanukia vizuri”

**Jack:** Ammm… ni viazi vya kuchemsha. Huo ndio upishi niliouzoea tu, na hata havijakuwa tayari.”

**OUTRO..**

(Mtangazaji):

Kwa kweli tangu hapo, hakuna mtu ambaye amemtaka Jack au Jenny kupika. Makala ya leo imeandikwa na Lydia Heller. Asante kwa kusikiliza na uwe mwangalifu ikiwa utataka kulijaribu zoezi hilo. Na iwapo unataka kusikiliza tena makala kwa mara myimgine kutaka kujifunza zaidi kuhusu masuala ya Sayansi, unaweza kufanya hivyo

kupitia mtandao wetu wa www.dw.de/kiswahili. Ni hayo tu tuliyoweza kukuandalia kwa hadi wakati mwingine-Kwaheri.

.